BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOJA YA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA KUDUMU ZA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

## (Imefanywa Chini Ya Kanuni Ya 145 Ya Kanuni Za Kudumu Za Baraza La Wawakilishi, Toleo La 2020)

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo ndani yake kwa kuturuzuku uhai na afya njema ambayo imetuwezesha leo hii kukutana hapa.

Aidha, nachukuwa nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Daktari Hussein Ali Mwinyi kwa kusimamia vyema amani ya nchi yetu na kutimiza azma yake ya kuwafikishia maendeleo wananchi tunaowaongoza.

**Mheshimiwa Spika,** naomba niendeleze shukurani zangu kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyotuongoza katika Baraza hili.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, nachukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah kwa juhudi kubwa anazochukuwa akiwa ni Msemaji Mkuu wa Serikali katika Baraza hili.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kukusanya maoni ya Wadau, Kamati yetu ilifanya mazungumzo na Kiongozi huyu na kutoa maoni yake kwa lengo la kuimarisha Kanuni hizi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kuwashukuru Mawaziri, Mwanasheria Mkuu, Naibu Mawaziri pamoja na Wajumbe wote wa Baraza kwa michango yao waliyoitoa wakati walipokutana na Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo Kamati inatambua michango ya wadau mbalimbali ambayo wameiwasilisha mbele ya Kamati wakiwa ni wataalamu na

wabobezi katika masuala ya Kanuni na taratibu za uendeshaji wa Mabunge.

Wadau wenyewe ni hawa wafuatao:

| NAM. | JINA | CHEO |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ibrahim Mzee Ibrahim | Jaji wa Mahakama Kuu Zanzibar na Katibu Mstaafu wa Baraza la Wawakilishi. |
| 2. | Mhe. Said Hassan Said | Jaji wa Mahakama Kuu Zanzibar na Mwanasheria Mkuu Mstaafu. |
| 3. | Dkt. Ali Ahmed Uki | Mkuu wa Skuli ya Sheria Zanzibar. |
| 4. | Ndugu Mussa Kombo Bakar | Katibu Mtendaji, Kamisheni ya Ardhi na Mkurugenzi Mstaafu wa Idara ya Shughuli za Baraza na Ushauri wa Kisheria Afisi ya Baraza la Wawakilishi. |
| 5. | Ndugu Mdungi Makame Mdungi | Afisa Mwandamizi kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Mkuu wa Utawala na Rasilimali Watu Mstaafu wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi. |
| 6. | Ndugu Saleh Said Mbarak | Mwanasheria wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo. |
| 7. | Ndugu Saleh Ali Salim | Mratibu Mstaafu wa Shughuli za Baraza la Wawakilishi - Pemba. |
| 8. | Ndugu Amour Mohammed Amour | Mkuu wa Utawala na Rasilimali Watu Mstaafu wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi. |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imetekeleza wajibu wake huo kwa kuzingatia masharti ya Katiba, Sheria na Kanuni za Baraza la Wawakilishi ili kuhakikisha kwamba Kanuni zinazotungwa haziendi kinyume na masharti hayo.

**Mheshimiwa Spika,** sababu kuu zilizopelekea kufanyika kwa marekebisho ya Kanuni hii ni pamoja na kukidhi mapendekezo ya Wajumbe, mabadiliko ya wakati na mahitaji ya kwenda sambamba na Mabunge mengine ya Jumuiya za Madola, pamoja na kuzirekebisha baadhi ya kanuni zinazoonekana kukwaza utendaji wa shughuli za Kamati na Baraza kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hayo, Baraza la Wawakilishi limeona kuna haja ya kutumia uwezo wake uliopewa na Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa

kuzifanyia marekebisho baadhi ya kanuni za Kanuni hizo ama kwa kuzifanyia marekebisho ya kawaida, kufuta, kufuta na kuziandika upya au kuongeza kanuni mpya ili kwenda sambamba na matukio na mabadiliko mbali mbali yaliyojitokeza Kitaifa na Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** naomba sasa nieleze kwa ufupi baadhi tu ya Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni kwa kuwa uchambuzi kamili wa Mapendekezo hayo umewekwa kwenye waraka ambao tayari Waheshimiwa Wajumbe mmeshawekewa kwenye vishikwambi.

**Mheshimiwa Spika,** katika Sehemu ya Kwanza Kamati imebaini kuwa katika kanuni ya 2 ya Tafsiri na Ufanunuzi kuna baadhi ya maneno yaliyotumika katika Kanuni hizo hayaakisi uhalisia uliopo, hivyo, hayawezi kutimiza dhamira iliyokusudiwa.

Kwa msingi huo, Kamati inapendekeza kufanyika mabadiliko ya tafsiri za maneno mbali mbali ili yaweze kutoa ufafanuzi uliokusudiwa kwa kukidhi haja ya Kanuni hizi. Katika kutekeleza hilo, Kamati imependekeza baadhi ya tafsiri kufutwa na kuandikwa upya, kufanywa marekebisho baadhi ya tafsiri ya maneno na pia kuongeza tafsiri mpya za maneno ambayo hayakuwepo awali.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa tafsiri mpya zilizoingizwa ni pamoja na tafsiri ya maneno: **"Kifaa cha elektroniki"**, **"Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza"**, **"Maslahi binafsi"** na kadhalika.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji wa shughuli za Baraza, Kamati imependekeza kufutwa na kuandikwa upya fasili ya (1) ya kanuni ya 15 inayohusiana na Mnadhimu wa Chama na kupendekeza kwamba ili Chama cha Siasa chenye Wajumbe ndani ya Baraza kuwa na Mnadhimu wa Chama ni lazima kwa Chama hicho kuwa na viti vya majimbo visivyopungua kumi.

Aidha, Kamati imependekeza kuongezwa fasili mpya ya (2) mara baada ya fasili ya (1) itakayoviruhusu Vyama vya Siasa kuungana ili vifikie kiwango kinachohitajika kama wataona kuna haja ya kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kwamba Muundo wa Utumishi wa Baraza la Wawakilishi unatambuliwa kikamilifu na Kanuni hizi, Kamati inapendekeza kuongezwa kanuni mpya ya 17 kuhusiana na Mkuu wa Divisheni ya Kamati na majukumu ya Mratibu wa Kamati ili Kiongozi huyo aweze kutambulika kikanuni kuwa ndio msimamizi wa shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza kuongezwa fasili mpya ya (1)(e) katika kanuni ya 19 inayowapa mamlaka Wapambe wa Baraza kuhakikisha kwamba

Mjumbe, Mtumishi na Mgeni anafuata na kutekeleza masharti yote yaliyoelezwa katika Kanuni hii kuhusiana na suala la mavazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imependekeza kuongezwa fasili hiyo kwa kuwa hivi sasa hakuna mhusika wa moja kwa moja anayesimamia suala la mavazi katika Baraza endapo Mjumbe, Mtumishi na Mgeni atavaa kinyume na masharti yaliyowekwa na Kanuni.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulitanabahisha Baraza lako kuwa, Kamati hii imependekeza kufanyiwa marekebisho kanuni ya 136(6)(a) inayohusiana na mavazi kwa Mjumbe mwanamke baada ya kuhisi kuwa kuna haja na Wajumbe hawa kuwekewa mavazi rasmi ya kuvaa katika kulinda hadhi na heshima ya Baraza hili. Hivyo, kufuatia mapendekezo hayo, Mjumbe mwanamke sasa atatakiwa atavaa kama ifuatavyo:

(i) suti kamili;

(ii) kitenge;

(iii) kilemba au mtandio kwa atakayependa; au

(iv) baibui la abaya siku ya Ijumaa kwa atakayependa

Isipokuwa kwamba, mavazi hayo yaliyoelezwa yanatakiwa kuwa:

(a) yenye mikono;

(b) yasiobana;

(c) yasiyoonesha maumbile ya mwili au nguo za ndani; na

(d) yanayofunika magoti.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imependekeza kufanyika marekebisho ya kanuni zinazohusu Nyakati za Vikao ambapo hapo awali shughuli za vikao vya Baraza zilikuwa zinafanyika mara mbili yaani asubuhi saa 3:00 kamili na kuendelea jioni saa 11:00 kamili.

**Mheshimiwa Spika,** dhamira kuu ya kufanya marekebisho hayo ni kuwawezesha Wajumbe kuweza kutekeleza majukumu ya Baraza kwa ufanisi pamoja na kwenda sambamba na nchi za Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Hivyo basi, Kamati inapendekeza kufanyika marekebisho ya kanuni ya 23 kwa kufutwa na kuandikwa upya na hivi sasa inapendekezwa shughuli za Baraza kuanza saa 3:00 kamili za asubuhi hadi saa 9:00 kamili za mchana, isipokuwa kwamba, siku za Ijumaa shughuli za Baraza zitaanza saa 3:00 asubuhi na kumalizika saa 6:00 mchana.

**Mheshimiwa Spika,** ili Baraza lako liweze kunyamazisha vilio vya Wajumbe wako vya kutojibiwa maswali yao ya nyongeza pale Mheshimiwa Waziri anavyoahidi kujibu

kwa maandishi maswali hayo. Kamati imependekeza kuongezwa fasili mpya ya (4), (5), (6) na (7) ya kanuni ya 40 kwa lengo la kuhakikisha kuwa maswali yote yaliyoahidiwa kujibiwa kwa maandishi yanapata majibu kwa wakati ili kuleta tija iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Baraza lako kuwa, kutokana na mapendekezo hayo mapya endapo Waziri husika atashindwa kujibu swali hilo kama alivyoahidi, Afisi ya Baraza itatoa taarifa hiyo kwa Mkuu wa Shughuli za Serikali katika Baraza kwa ajili ya kuchukua hatua zaidi na endapo bado maswali hayo hayakujibiwa ndani ya siku tano za kazi, Mheshimiwa Spika atatoa taarifa ya kutokujibiwa mswali hayo mbele ya Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuondosha utata juu ya masuala yepi yanayopaswa kuwasilishwa mbele ya Baraza kama ni Kauli ya Serikali au Taarifa ya Serikali, Kamati imependekeza kufanyiwa marekebisho kanuni ya 43 na 44 kwa kuyataja maeneo yanayopaswa kuwa Kauli ya Serikali na yale yanayopaswa kuwa Taarifa ya Serikali,

**Mheshimiwa Spika,** maeneo yaliyopendekezwa kuwasilishwa kama ni Kauli ya Serikali ni pamoja na:

(a) Sheria za Muungano zitakazopelekwa mbele ya Baraza kwa mujibu wa kifungu cha 132 cha Katiba;

(b) Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali itakayowasilishwa ndani ya Baraza chini ya kifungu cha 112 cha Katiba;

(c) Majanga au matukio ambayo yataleta athari kwa jamii; au

(d) Jambo jengine lolote ambalo Serikali linawajibika nalo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Taarifa ya Serikali, Kamati inapendekeza maeneo yafuatayo yawasilishwe kama ni Taarifa hiyo:

(a) Taarifa ambayo Sheria husika imeelekeza;

(b) Taarifa ya jambo lolote ambalo lilichunguzwa;

(c) Taarifa kuhusiana na Utekelezaji wa Serikali juu ya:

(i) Maazimio ya Hoja ya Mjumbe,

(ii) Maazimio ya Kamati Teule,

(iii) Maazimio yoyote ya Baraza ambayo Serikali inatakiwa kuwasilisha Taarifa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(d) Jambo jengine lolote ambalo Serikali linawajibika nalo.

**Mheshimiwa Spika,** kanuni ya 59 inapendekezwa kufanyiwa marekebisho katika

fasili ya (6) inayohusiana na muda wa Wajumbe kuchangia katika Baraza, ambapo inapendekezwa Mjumbe kuzungumza kwa muda usiozidi dakika kumi na tano katika mikutano ya kawaida na dakika ishirini wakati wa mikutano ya bajeti, isipokuwa kwamba, Mheshimiwa Spika akiona inafaa anaweza kuongeza au kupunguza muda usiozidi dakika tano.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la mapendekezo hayo ni kuwapatia Wajumbe muda wa kutosha wa kuchangia katika mikutano ya Kawaida na ya Bajeti ili kuweza kuwawakilisha vyema wananchi waliowachagua ndani ya Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo imebaini kuwa baadhi ya Wajumbe na Wageni wanaoingia katika ukumbi wa Baraza wanatumia kifaa cha kielekrtoniki kama vile simu kinyume na masharti ya kanuni ya 62(2) ya Kanuni hii. Hivyo, Kamati inapendekeza kufutwa na kuandikwa upya fasili ya (2) ya kanuni hiyo ili iwe kanuni mpya mara baada ya kanuni ya 62 kwa lengo la kudhibiti matumizi bora ya kifaa hicho.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mnasaba huo, tumependekeza kanuni hiyo itowe ruhusa kwa Mjumbe au mtu mwengine yeyote kuingia na kutumia kifaa cha kielektroniki ndani ya Baraza endapo atapenda isipokuwa kwamba, ahakikishe kuwa;

(a) kifaa hicho hakitoi sauti;

(b) hakiingilii mawasiliano ndani ya Baraza;

(c) hakitumiki kwa mazungumzo;

(d) hakitoleta madhara yoyote ndani ya Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** naomba uniruhusu niielezee aya ya (c) kwa msisitizo wake kwani hivi sasa baadhi ya Wajumbe na Wageni wanaoingia katika ukumbi wa mkutano wa Baraza wanatumia sana simu kwa kuzungumza huku mijadala ndani ya Baraza ikiendelea. Mheshimiwa Spika, naomba ifahamike kuwa kitendo hicho ni kwenda kinyume na Kanuni za Baraza na endapo Mjumbe au Mgeni atavunja sharti hilo anaweza kuchukuliwa hatua chini ya kanuni hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo imependekeza kufanyiwa marekebisho kanuni ya 75 inayohusiana na Mahudhurio katika Baraza na Kamati zake. Mheshimiwa Spika, Kamati hii imependekeza Mjumbe wa Baraza kulipwa posho ya kikao cha siku pamoja na posho la kujikimu kama itakavyoamuliwa na Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza, ambapo posho ya kikao cha siku itatolewa tu kwa Mjumbe aliyehudhuria kikao na kusaini mahudhurio.

Kwa mantiki hiyo, Mjumbe atakayeshindwa kuhudhuria kikao cha Baraza hatolipwa posho la kikao cha siku hiyo, isipokuwa kwamba, endapo Mjumbe hakuridhika na

uamuzi uliofanywa na Mheshimiwa Spika wa kukatwa posho hilo anaweza kuwasilisha lalamiko lake kwa Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** kwenye Proviso ya fasili ya (3) ya kanuni hiyo, Kamati imependekeza iwe fasili mpya ya (5) mara baada ya fasili ya (4) na fasili zinazoendelea zitafuata mpangilio huo. Mheshimiwa Spika, katika fasili hiyo Kamati imependekeza kuongezwa aya mpya ya (c) ambayo inaruhusu Mjumbe mwanamume kupatiwa siku 3 za mapumziko endapo mwenza wake atajifungua isipokuwa kama mtoto aliyezaliwa atafariki. Lengo la kupendekeza hilo pamoja na mambo mengine ni kumpatia Mjumbe nafasi ya kuihudumia familia yake kwa karibu zaidi katika kipindi hicho.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 88(a) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Baraza la Wawakilishi ndio chombo kikuu chenye jukumu la kutunga sheria zisizohusiana na masuala ya Muungano, hata hivyo, Baraza la Wawakilishi limekasimu madaraka yake ya kutungwa Kanuni kwa Serikali. Pamoja na hayo, Baraza limebaini shughuli hiyo iliyokasimiwa haitekelezwi ipasavyo na kupelekea baadhi ya Sheria zinazotungwa kutotekelezeka kutokana na kutokuwepo kwa Kanuni husika.

**Mheshimiwa Spika,** ili kutatua changamoto hiyo, Kamati hii inapendekeza kuongezwa fasili mpya ya (2) ya kanuni ya 83 ambayo italazimisha Mswada wowote utakaowasilishwa katika Baraza kuambatanishwa na Rasimu ya Kanuni husika na endapo Rasimu hiyo haijakamilika basi Rasimu husika iwasilishwe kwa Spika ndani ya miezi sita.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuwa na utekelezaji bora wa shughuli za Baraza, Kamati hii imependekeza kuongezwa kanuni mpya mara baada ya kanuni ya 95 itakayompa mamlaka, Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza au Waziri anayehusika na Wizara hiyo kuwasilisha utekelezaji wa Bajeti wa mwaka uliopita wa Serikali pamoja na kupewa mamlaka Waziri anayehusika na Wizara hiyo kuwasilisha na kutoa hoja ya Makadirio ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la pendekezo hilo ni kutoa nafasi kwa Wajumbe wa Baraza kuhoji kikamilifu utekelezaji wa bajeti wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwani imebainika kuwa hivi sasa Wajumbe hawapati fursa ya kuichangia kwa uwazi zaidi bajeti ya Ofisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kanuni ya 98 Kamati imependekeza kuongezwa siku za kujadili bajeti ya Serikali, ambapo badala ya siku 35 imependekezwa kuwa iwe siku 40, isipokuwa kwamba, zinaweza kuongezwa siku zisizozidi 5. Mheshimiwa Spika, Kamati imependekeza hilo kwa lengo la kutoa nafasi ya kutosha kwa Wajumbe katika kuchangia bajeti kwani kitendo cha Baraza kubadilisha muda wa vikao vyake

kumepelekea kupungua kwa dakika arobaini na tano kwa kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imependekeza kuongezwa fasili mpya ya (3) mara baada ya fasili ya (2) ya kanuni ya 95 inayohusiana na uwasilishaji wa Bajeti Kuu ya Serikali, ambapo, inapendekezwa kuwa Waziri anayehusika na mambo ya Fedha kuwasilisha Bajeti hiyo kwenye Baraza katika wiki ya pili ya mwezi wa Juni ili Zanzibar iweze kwenda sambamba na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo imebaini kuwa fasili ya (6) ya kanuni ya 137 inayohusiana na uwasilishaji wa Ripoti ya Wajumbe watano wanaochaguliwa na Baraza kuingia Bungeni haipo wazi. Hivyo, ili kuondosha kasoro hiyo, Kamati imependekeza Wajumbe hao kuwasilisha tu Ripoti ya mrejesho wa Azimio lililotolewa na Baraza na sio vyenginevyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo imependekeza kufutwa na kuandikwa upya kanuni ya 147 ambapo katika fasili ya (4) ya kanuni hiyo, Kamati imependekeza Spika, Naibu Spika, Waziri au Naibu Waziri kutokuwa Mwenyekiti, Makamo Mwenyekiti, Katibu au Mshika fedha wa Jumuiya au klabu yoyote iliyoanzishwa na Baraza ili kuwapa muda wa kutosha viongozi hao katika kutekeleza majukumu yao ya Kitaifa.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo yangu hayo, naomba sasa nieleze kwa ujumla baadhi ya mambo yaliyojitokeza wakati Kamati hii inapokea maoni ya Wadau ambayo kwa hivi sasa hatukuweza kuyafanyia kazi hadi hapo hatua nyengine zitakapochukuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa mapendekezo hayo ni pamoja na kuongezwa baadhi ya watu kuwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza. Watu wenyewe ni hawa wafuatao:

(i) Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu;
(ii) Mheshimiwa Waziri anayehusika na masuala ya Fedha; na
(iii) Mheshimiwa Waziri anayehusika na Utumishi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hii inakubaliana na pendekezo hilo na inaishauri Afisi ya Baraza la Wawakilishi kuifanyia marekebisho Sheria ya Utawala wa Baraza Nambari 6 ya mwaka 2019 kwa kuwa Muundo wa Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza umeelezwa kwenye Sheria hiyo ili waongezwe Wajumbe hao muhimu kwa maslahi ya Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, katika kupitia nyaraka mbalimbali za Sheria

pamoja na Katiba ya Zanzibar, Kamati hii imebaini kuwa vifungu vya 66 na 119 vya Katiba vinatambua kuwepo kwa nafasi ya Kiongozi wa Upinzani ndani ya Baraza nafasi ambayo haitambuliki kikanuni kufuatia Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (GNU) uliopo hapa Zanzibar tokea mwaka 2010.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mantiki hiyo, Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo inaiomba Serikali kuvifanyia marekebisho vifungu hivyo vya Katiba ili kuondosha utata uliopo.

**Mheshimiwa Spika,** sasa naomba kuchukuwa fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe kwa kuniruhusu kusimama hapa ili niwasilishe Hoja ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo kuhusu Marekebisho ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Toleo la 2020.

**Mheshimiwa Spika**, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao makubwa waliyonipa na kuweza kuandaa Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni hizi na leo hii nimeweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu, kwani halikuwa jambo la rahisi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba uwatambue Wajumbe hawa kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:

| NAM. | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mihayo Juma Suleiman N'hunga | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | Mjumbe |
| 4. | Mhe Suleiman Masoud Makame | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Hassan Hamad Omar | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Yussuf Hassan Iddi | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** shughuli za Kamati hii zimekuwa zikiratibiwa na Makatibu wawili kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi, naomba nitambue mchango wao katika kufanikisha kazi hii. Makatibu hao wamekuwa ni msaada mkubwa na mafanikio ya Kamati hii.

Naomba nao niwataje kwa majina yao kama ifuatavyo:

| NAM. | JINA | WADHIFA |
| --- | --- | --- |
| 1. | Ndg. Karima Abdul- Wahab Alawy | Katibu |
| 2. | Ndg. Noman Thabit Noman | Katibu |

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio mwisho kwa umuhimu, naomba kumshukuru kwa dhati kabisa Katibu wa Baraza la Wawakilishi – Ndg. Raya Issa Msellem, Mkurugenzi wa Idara ya Shughuli za Baraza, Mkurugenzi wa Idara ya Ushauri wa Kisheria, Wanasheria wa Afisi ya Baraza, na Watendaji wote wa Baraza kwa mashirikiano yao makubwa waliyoipatia Kamati hii wakati wote ilipokuwa inatekeleza shughuli hii.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na maelezo yangu yote niliyoyatoa naomba kuhitimisha shughuli hii kwa kuliomba Baraza la Wawakilishi kwa kutumia uwezo lililopewa na kanuni ya 145(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020 kupitisha Azimio la kuzifanyia marekebisho Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020, kwa lengo la kutimiza hoja nilizozieleza, sambamba na kuwaomba Wajumbe wa Baraza hili kujadili na kuchangia ipasavyo Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni niliyowasilisha pamoja na marekebisho mengine yoyote ya Kanuni hizi kama yapo na hatimae kuzipitisha ili kuwa na Kanuni zitakazokidhi haja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

……………………………

**Mihayo Juma N'hunga**
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO,**
**BARAZA LA WAWAKILISHI,**
**ZANZIBAR.**